**KIKAO CHA TATU CHA MTAA WA KILOMBERO 2026**

May 10, 2026 sunday

Wajumbe

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mumbara Peter Mumbara | Mwenyekiti |
| 2. | Abdon Godfrey | Katibu |
| 3. | Angel wabeya | Mjumbe |
| 4. | Peter magoti | Mjumbe |
| 5. | Simon kinyonyi | Mjumbe |
| 5. | Wema mbwambo | Mjumbe |
| 6. | Isaya mwera | Mjumbe |
| 7. | Grace obadia | Mjumbe |
| 8. | Grace bigambo | Mjumbe |
| 9. | Godwin kabogo | Mjumbe |
| 10. | Alphaxade joshua | Mjumbe |
| 11. | Mwanaidi msuya | Mjumbe |
| 12. | Edson kinyika | Mjumbe |
| 13. | Michael Allen | Mjumbe |
| 14. | Frank Method | Mjumbe |
| 15. | Ester Mpare | Mjumbe |

**AGENDA**

1.Kufungua kikao.

2.Nyumba ya mchungaji.

3.Uzinduzi wa begi la mtoto na sanduku la sadaka.

4.Njombe net event.

5.Uaminifu.

6.Taarifa ya idara ya huduma wanawake kila mwezi.

7.Semina za watoto.

8.Dodoso idara ya huduma za wanawake.

9.Vitabu vya utume.

10.Vitabu vya uwakili.

11.Katibu wa A.M.R wa mtaa.

12.Katibu msaidizi wa mtaa.

13.Kufunga kikao

**1.Kufungua kikao**

- Kikao kilifunguliwa mnamo saa 05:15 asubuhi ombi la ufunguzi kutoka kwa grace obadia kutoka kanisa la kidatu.

**2.NYUMBA YA MCHUNGAJI**

- Taarifa ni kwamba kamati ya ufuatiliaji nyumba ya mchungaji ambao ni viongozi wa majengo makanisani kati yao amechaguliwa ndugu julius mashauri kuwa mwenyekiti na katibu wake ni fredi felix.

**3.UZINDUZI WA BEGI LA MTOTO NA SANDUKU LA SADAKA.**

- Utekelezaji wa uzinduzi wa begi la mtoto na sanduku la sadaka utakuwa kama ufuatavyo makanisani chini ya usimamizi wa mchungaji wa mtaa akiwepo katika uzinduzi huo,
- Kanisa la kidatu litafanya uzinduzi huo tarehe 16/05/2026
- Upande wa nyamvisi, kidodi na kitete watafanya pamoja siku ya tarehe 20/06/2026
- Kanisa la mkamba litafanya uzinduzi huo wa begi la mtoto na sanduku la sadaka tarehe 27/06/2026
- Kanisa la kilombero watafanya uzinduzi tarehe 18/07/2026
- CHA KUZINGATIA KIONGOZI WA WATOTO AWE ANASHIRIKIANA NA MHADHINI KATIKA KUWEKA KUMBUKUMBU ZA MATOLEO YA WATOTO.

## 4.NJOMBE NET EVENT

- Kuhusu mkutano wa njombe net event tunatakiwa kutoa taarifa za kituo mapema kwa mchungaji kwa wale wote walioandaliwa kwaajili ya ubatizo na pia kushiriki kutoa taarifa kwa namba za mawasiliano zinazotolewa katika mkutano kwaajili ya kutoa taarifa za vituo vilivyowekwa makanisani na hata vya majumbani kwa washiriki binafsi.
- Kilombero sda church wanavituo vitatu wanavyosimamia.
- Nyamvisi sda church vituo viwili.
- Mkamba sda church vituo viwili.
- Kidatu sda church kituo kimoja.
- Kidodi sda church kituo kimoja.

## 5.UAMINIFU

- Taarifa ya orodha ya kila mwezi ya waaminifu katika matoleo zaka na sadaka, wazee na wahadhini wanaombwa kutoa ushirikiano kila mwezi kutoa takwimu ya makanisa yao, matoleo kwa watoto na watuwazima.

## 6.TAARIFA YA IDARA YA HUDUMA WANAWAKE KILA MWEZI.

>Taarifa kutoka uongozi wa idara ya wanawake konferensi ni kwamba wanaitaji taarifa ya kila mwezi kutoka makanisani ya idara ya wanawake, hivyo viongozi wa idara ya wanawake makanisani wazingatie kujaza taarifa husika.

## 7.SEMINA ZA WATOTO

- Kuhusu semina ya watoto kutakuwa na semina tarehe 15-17/05/2026 eneo la morogoro,
- ifakara tarehe 22-24/05/2026
- CHAKUZINGATIA katika semina hizo majina ya watoto wawasilishe mapema wanaokwenda pia, ambao hawatahudhuria hawata pewa nafasi katika kufundisha, pia walimu watatoka kwenye konferensi yetu tu.

## 8.DODOSO IDARA YA HUDUMA ZA WANAWAKE

- Kuhusu dodoso ya taarifa inapaswa kujazwa na kila mhusika wa idara ya wanawake kanisani mmoja mmoja nasi mkuu wa idara kuwajazia washiriki wengine na idara ina husu wale kuanzia umri miaka 15 kuendelea hao ndio wanaingia katika idara ya huduma ya wanawake, hivyo taarifa zijazwe na kutumwa kwa mchungaji kuhusu dodoso za idara hii ya huduma za wanawake.

**<u>9.VITABU VYA UTUME</u>**

>Taarifa ni kwamba kila kanisa linapaswa kuhakikisha linanunua vitabu vya utume MANENO YA MATUMAINI,
>Kuhusu swala la kuvipata vitabu makanisa yamerahisishiwa kuvipata vitabu kwa kutuma pesa katika account zifuatazo kupata huduma hii
> CRDB 0150202380600 JINA SDA HOME HEALTH SERVICE
>NMB 23210000945 JINA SDA HOME HEALTH SERVICE
>KUZINGATIA, baada ya kulipia pesa hakikisha unafanya mawasiliano kuthibitisha malipo kwa kupitia namba hii 0791231288 pia kumbuka kumtumia risiti ya malipo uliyofanya kupitia account hizo.

**<u>10.VITABU VYA UWAKILI</u>**

- MAELEKEZO, kuhusu vitabu hivi vya uwakili ni muhimu makanisa kuwa navyo pia vinapaswa kusomwa na washiriki majumbani pia kutumika kama masomo kila siku za jumatano ya maombi visomwe na kujadiliwana na washiriki, vitumike katika siku ya kufungua sabato ijumaa, pia sabato mchana visomwe na kujadiliwana kwa maswali na majibu kwa yale yatakayoulizwa kulingana na somo lilivyoendeshwa siku iyo. Makanisa yazingatie hilo ni muhimu kwaajili kuwafanya washiriki wawe mawakili wema.

**<u>11.KATIBU WA AMR MTAA</u>**

Katibu wa mtaa wa AMR aliyependekezwa ni ndugu FURAHA GODWIN kutoka kanisa la kilombero.

**<u>12.KATIBU MSAIDIZI WA MTAA</u>**

Wajumbe wamempendekeza ndugu UPENDO JOHN kuwa katibu msaidizi mtaa.

**<u>13.Kufunga kikao</u>**

Kikao kilifungwa mnamo saa 12:40 mchana na ombi la kufunga kikao lilitolewa na SIMON KINYONYI.